BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 24 Septemba, 2024**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Ripoti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

142. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

(a) Kwa kiasi gani viongozi wa dini wanatoa mchango katika kupambana dhidi ya madawa ya kulevya nchini.

(b) Je, Serikali inashirikiana vipi na viongozi wa dini katika mapambano dhidi ya madawa hayo.

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

157. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

Tathmini iko vipi juu ya mafanikio ya Idara ya Diaspora mpaka hivi sasa.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

30. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo miradi ya ujenzi wa barabara mbali mbali licha ya kujitokeza kwa changamoto kadhaa katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Je, ni sababu zipi zinazomkwamisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuifanyia ukaguzi miradi hiyo wakati inaendelea (Real Time Audit).

139. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

(a) Ni sheria zipi ambazo zinamlinda mtoa taarifa dhidi ya vitendo vya uhujumu wa uchumi na rushwa.

(b) Kwa kiasi gani sheria hizo zimekuwa zikisaidia na kupunguza vitendo vya rushwa nchini.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

13. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Imekuwa ni kawaida kwa Serikali kufanya uhakiki wa madeni yake kabla ya kulipa madeni hayo kwa lengo la kujiridhisha na madai hayo. Kwa kuwa mchakato wa uhakiki wa madeni ya wakandarasi na watoa huduma mbali mbali katika taasisi za Serikali umekamilika.

Je, ni kiasi gani cha deni hilo limeonekana ni halali kulipwa na ni kiasi gani sio halali kulipwa.

14. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Moja kati ya changamoto ya ukusanyaji wa kodi kwa wafanyabiashara wakubwa ni kesi za kikodi.

Je, kwa kiasi gani kesi za kikodi zinaathiri ukusanyaji wa mapato hapa Zanzibar.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

101. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Licha ya jukumu kubwa la vikosi vyetu vya Idara Maalum vya SMZ kulinda amani na utulivu wa nchi yetu.

Je, ni ipi nafasi ya jeshi hilo katika kushiriki kwenye harakati za kukuza uchumi na kujenga taifa letu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

76. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika eneo la Nyumba Mbili Mwanakwerekwe kuna kijana amekuwa akijitolea mvua jua kuongoza utaratibu wa gari na raia kuvuka kwa usalama.

Je, Serikali inamuangalia kwa jicho gani la huruma kijana huyu mzalendo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

261. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli nyingi za msingi na sekondari zinatumia mfumo wa kuandaa mitihani kwa kutumia karatasi ili kuongeza ufanisi na ufaulu kwa wanafunzi. Hata hivyo, skuli hizi zina mahitaji makubwa ya mashine za kuchapishia na kutolea kopi, huku mashine hizo zikikosekana. Jambo hili linakwamisha utendaji wa skuli nyingi zilizopo Unguja na Pemba.

(a) Kwa kiwango gani Serikali inalitambua tatizo hili na hatua zipi imezichukua ili kulitatua.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha usambazaji na matengenezo ya vifaa vya ofisi kama mashine za kuchapishia ili kupunguza athari za ukosefu wa vifaa hivi.

(c) Je, Serikali inafahamu changamoto za kifedha zinazozikabili skuli katika ununuzi wa vifaa na karatasi za kuchapishia (rim papers) na kuna mpango gani wa kutoa msaada wa kifedha kwa skuli zinazokumbwa na upungufu huu.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

121. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(b) Ni tuzo gani maarufu za kimataifa ambazo wasanii nguli wa muziki wa taarabu asilia wamefanikiwa kuzipata akiwemo bwana Moh'd Ilyas.

(b) Ni kwa kiasi gani mafanikio hayo yanatambuliwa nchini na kupewa heshima yake kubwa.

(c) Nini matarajio ya kuwawekea kumbukumbu za kudumu wasanii hawa wakongwe wanaoudumisha utamaduni wetu kupitia muziki wa taarab asilia.

122. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kiasi gani wasanii nguli wa tasnia ya sanaa ya muziki na maigizo wanatumika ipasavyo katika kuuendeleza utamaduni wa sanaa ya muziki na maigizo ya kizanzibari kupitia Wizara yako.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

268. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Yapo malalmiko ya uharibifu wa mazingira kwa wauzaji wa vyakula katika eneo la Forodhani. Wauzaji wengi wanatupa baadhi ya mabaki ya vyakula katika fukwe, jambo linalopelekea uharibifu wa eneo hilo la kitalii.

(a) Je, kwa kiwango gani Serikali inalitambua tatizo hilo na kwa kiasi gani inalishugulikia ili kulinda haiba na mandhari ya Forodhani.

(b) Je, ni upi mkakati wa Serikali katika kuliboresha zaidi eneo la Forodhani ili liwe la kisasa na kuzidi kuvutia wageni.

(c) Je, ni mapato ya kiasi gani hupatikana kwa mwaka katika eneo hilo la Forodhani.

**Wizara ya Afya:**

81. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tathmini iko vipi juu ya uwepo wa madaktari wa kike kwa ajili ya kutoa tiba hususani kwa maradhi maalumu yanayowahusu kinamama.

230. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha Afya cha Chukwani ni miongoni mwa vituo vinavyotoa huduma masaa ishirini na nne lakini kwa masikitiko makubwa, kuna uhaba mkubwa wa vitendea kazi na hakuna madaktari kwa muda wote.

(a) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuzitatua changamoto hizo.

(b) Je, ni lini Serikali itaipatia ufumbuzi changamoto ya uhaba wa vitendea kazi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

244. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi za kuendeleza miradi ya nishati mbadala. Katika juhudi za kutafuta vyanzo vya nishati endelevu, matumizi ya umeme kutokana na maji ya chumvi (sea water current) yanaweza kuwa suluhisho muhimu kwa nchi yetu.

(a) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti juu ya uwezekano wa kutumika maji ya bahari katika kuzalisha umeme.

(b) Je, Serikali ina mipango gani ya kutumia teknolojia ya umeme inayotokana na maji ya bahari ili kuongeza uzalishaji wa umeme na kupunguza utegemezi kwenye vyanzo vya nishati vya jadi.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

### Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2023/2024.

### Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2023/2024.

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**

**Zanzibar,**
**24 Septemba, 2024.**